



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO**

**TAARIFA KWA UMMA
FURSA ZA AJIRA KWA MAFUNDI KATIKA NCHI YA
UMOJA WA FALME ZA KIARABU**

Dodoma, 27 Oktoba 2026

Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano kwa kushirikiana na Kampuni ya Target Tours and Labour Supply Limited inapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa stahiki kutuma maombi kwa ajili ya kujaza nafasi 470 za Mafundi Ujenzi zilizotolewa na Kampuni ya DHCN General Construction L.L.C – S.P.C ya nchini UAE – Abu Dhabi kama inavyoelezwa hapa chini: -

1. MAELEZO YA FURSA ZA AJIRA

Aina ya kazi	Idadi ya nafasi
Fundi Rangi (Painter)	30
Fundi Mchundo (Steel Fixer)	50
Fundi Seremala (Carpentry)	50
Fundi Bomba (Pipe Fitter)	80
Msaidizi wa Fundi (Helper)	120
Fundi Viunzi (Scaffolder)	80
Fundi Uchomeleaji (Welder)	60
Jumla	470

Mwajiri: DHCN General Construction L.L.C – S.P.C

Mahali pa kazi: Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)

Umri: Miaka 21–45

Aina ya ajira: Mkataba wa miaka miwili, unaoweza kuhuishwa.



www.kazi.go.tz

ofisi_ya_waziri_mkuu_kazi

Kazi Online TV

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Kazi,
S.L.P 2890, 40411 DODOMA.
Barua pepe: ps@kazi.go.tz,
Hotline: 026-296350

2. SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na elimu ya msingi au sekondari.

Awe na uzoefu wa mwaka mmoja na zaidi katika fani ya Ufundi Rangi, Mchundo, Seremala, Bomba, Viunzi na Uchomeleaji;

Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya Kiingereza.

Awe mwanaume.

Awe na umri wa miaka 21 hadi 45.

3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Mshahara utalipwa kulingana na Sheria za nchi ya UAE;

Gharama za matibabu kwa kipindi chote cha ajira zitakuwa juu ya mwajiri;

Mwajiri atagharamia visa;

Mwajiri atagharamia tiketi ya kurudi baada ya kumaliza mkataba wa miaka miwili;

Mwajiri atagharamia malazi na chakula katika kipindi cha miaka miwili na;

Mwajiri atalipa gharama za usafiri wa kutoka nyumbani hadi kituo cha kazi kwa kipindi chote cha ajira.

4. MUDA WA KUTUMA MAOMBI NA TAREHE YA USAILI

Tarehe za kutuma maombi: 27 Oktoba – 3 Novemba 2026.

Tarehe ya usaili: 9, 10 na 11 Novemba 2026.

Mahali pa usaili: VETA, Dar es Salaam.

5. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wanatakiwa kutuma wasifu binafsi (Curriculum Vitae – CV) kupitia mojawapo ya njia zifuatazo: Tovuti: <https://www.targettours.co.tz> au Barua pepe: info@targettours.co.tz

Baada ya kutuma maombi, waombaji wanapaswa kujisajili kupitia mfumo wa Kazi Portal kwa kutumia kiungo hiki: <https://jobs.kazi.go.tz>

6. MAWASILIANO KWA MAULIZO

Kwa maelezo zaidi, piga simu kupitia namba zifuatazo:

+255 766 712 222

+255 781 801 818

+255 781 801 817

IMETOLEWA NA:

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI



www.kazi.go.tz

ofisi_ya_waziri_mkuu_kazi

Kazi Online TV

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Kazi,
S.L.P 2890, 40411 DODOMA.
Barua pepe: ps@kazi.go.tz,
Hotline: 026-296350